- Roho Mtakatifu humweka huru Mkristo kutoka katika sheria ya dhambi na kifo.-Warumi 8:2
- Roho Mtakatifu humuimarisha Mkristo kwa kumpa nguvu toka utu wa ndani – Waefeso 3:16
- Roho Makatifu humweka huru Mkristo katika kushuhudia. Matendo: 8

4. Ukamilifu na Matunda ya Roho Mtakatifu

- Wakristo wote ni lazima kujazwa na Roho Mtakatifu. Waefeso 5:18
- Matunda ya Roho Mtakatifu ni Upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, imani, kiasi. Wagalatia 5:22, 23
- Kusudi la Roho Mtakatifu ni kushirikisha neno la Mungu kwa ujasiri-Matendo 4:29, 31

5. Sifa za kujazwa na Roho Mtakatifu

- Mtu awe ameokoka. -Matendo 2:38
- Mtu lazima akiri dhambi zake anazozijua katika maisha yake-IYohana1:9 (Soma Zaburi 66:18)
- Kwa Imani, mwombe Roho Mtakatifu akujaze na kukuongoza-IYohana 5:14-15. (Soma warumi 1:17)
- Mtii Mungu kwa kila saa ya kila siku.-Matendo 5:32

Biblia inatupa kielelezo cha maana ya kujazwa na kuongozwa na Roho Mtakatifu katika utu wa Daudi. Tunaweza kuzitumia kweli NNE za kiroho zifuatazo na kumruhusu Mungu atuongoze na kututumia katika ufalme wake.

1. **<u>I Samweli 16:13 –</u> Nguvu ya kuishi maisha yaliyojawa na Roho Mtakatifu hutoka kwa Mungu**. Kama vile Mungu anavyowawezesha waumini leo hii, Daudi aliwezeshwa sana na Roho wa Mungu kwa sababu Mungu alikuwa na kusudi la kukamilisha katika maisha ya Daudi. Mungu anamakusudi na mpango katika maisha yako na Roho wake ndiyo nguvu inayoweza kukamilisha makusudi hayo. Nguvu haitokani na pesa, elimu, au nafasi nzuri wala Washington Dc lakini ni kwa Roho wa Mungu tu.

2. **<u>I Samweli 17:45 –</u> Kuwa na Mungu inatosha na hatuhitaji kitu kingine zaidi.** Goliathi alikuwa ameandaliwa. Alikuwa mpana, shupavu, mzoefu na silaha kwa ajili ya vita. Vipi kuhusu Daudi? Hakuwa mnene wala mpana au mtu mwenye nguvu. Hakuwa na silaha maalumu za vita na wala uzoefu katika vita. Daudi alikuwa hajawahi kupigana vita kama hii tangu azaliwe. Lakini Daudi alisema, "… Ninakuja kwako kwa jina la Bwana mweza Mungu wa jeshi la Israeli ambaye umekwisha mtukana." Yote aliyokuwa nayo Daudi ni Roho Mtakatifu na yote Daudi aliyoyahitaji!! na hiyo ndiyo wote tunahitaji! Mungu anapotuita tumfuate anatupa maono mapana ambayo hatuyawezi. Roho wake aliyeko ndani yetu anatosha na yeye ndiye .atafanya yale yote tunayoyahitaji.

3. **<u>I Samweli17:50 –</u> Mungu anataka kufanya yasiyowezekana kwa wanadamu kupitia sisi**. Nani alishinda? Hapana, Daudi hakushinda kwa sababu lilikuwa ni jambo lisilowezekana kwakwe. Mungu alishinda. Mungu anataka kufanya yale anayayotaka kufanya kupitia sisi. Anataka kufanya yasiyowezekana kwa manufaa yaliyo katika maeneo matatu:
    - **a.** Ndani yetu: Ni Mungu anaweza kuyageuza maisha yetu. Anataka kufanya yasiyowezekana ndani yetu. Anataka atugeuze tuwe kama vile Mungu alivyo, kitu ambacho ni kigumu sana kwetu.
    - **b.** Kupitia Sisi: Ni Mungu mwenyewe anaweza kufanya huduma yake. Anataka afanye huduma yake kupitia kwetu kitu ambacho ni kigumu kwetu sisi kukifanya.
    - **c.** katika roho za waliopotea: Ni Mungu awezae kuwaokoa waliopotea sisi hatuwezi. Mungu kwa Roho wake anatenda katika Roho za waliopotea ili apate kuwaonesha dhambi zao, awafunulie ile kweli ambayo itawaleta katika wokovu.

4. **<u>I Samweli 17:46 –</u> Mungu anatenda yasiyowezekana ili ulimwengu ufahamu kwamba yeye ni Mungu.** Kwa sababu Mungu hufanya yasiyowezekana, kwa kutumia watu wasio na ufahamu na hata watu ambao ni wachanga kabisa kila mtu alifahamu kwamba kulikuwa na nguvu kubwa kuliko hata Daudi. “kwamba kuna Mungu wa Israeli”. Kwa sababu ya nguvu kuu Mungu aliyoifunua Wafilisti waliogopa. Tunapomrushusu Mungu atende kazi katika maisha yetu anaweza kudhihirisha nguvu yake na watu wote wanaotuzunguka watafahamu kwamba kuna Mungu.

HITIMISHO

Unaposoma sehemu hii tunakuhimiza kuiangalia kwa makini mistari ifuatayo na umruhusu Roho Mtakatifu aseme nawe kupitia mistari hiyo.

Wakristo wana Roho Mtakatifu kwa njia ya Upako (I Yohana 2:20, 27; II Wakorintho 1:21), alama ya Muhuri (II Wakorintho 1:22; Waefeso 1:13), alama ya kuhifadhiwa (II Wakorintho 1:22; Waefeso 1:14), Alama ya ubatizo (I Wakorintho 12:13a) na alama ya kinywaji (I Wakorintho 12:13b; Yohana 4:14, 7:37-39a).

Tunapaswa kumtii yeye aliyetuambia “Enendeni ulimwenguni mkahubiri injili kwa kila kiumbe (Marko 16:15).” Tunapaswa kuyapenda maneno yake kwa sababu tumekwisha kutakaswa kwa njia yake (Yohana 17:17).

Tunapaswa kutenda kazi katika shamba la Bwana kwa ujasiri na furaha kwa sababu atatenda kazi pamoja nasi (Wafilipi 1:6; 2:13). Hakuna mapungufu ya karama kwa Wakristo (I Wakorintho 1:7). Roho Mtakatifu atatuwezesha kuwa na ibada ya Bwana na anafanya hii kwa sababu ya Karama alizoziweka ndani yetu (I Wakorintho 12:4-6).

Tunapaswa kumtii Mungu kadri tunavyozidi kuelewa Neno lake. Kwa kufanya hili matokeo yatakuwa ni matunda kutoka kwake yeye anayetenda mapenzi ya Mungu ndani yetu (Wagalatia. 5:22-26).

JINSI YA KUFANYA

- Omba kimya kimya.
- Mwombe Roho Mtakatifu akuoneshe dhambi iliyoko katika maisha yako.
- Ungama dhambi, zilizo katika akili zako.
- Jitoe kwakwe na umtii.

II. <u>MWINJILISTI MASHUHURI NA MAOMBI</u>

UTANGULIZI

Ni vigumu kuwa mwanafunzi wa Yesu bila kuwa mtu wa maombi. Mwinjilisti anapaswa kuwa na muda binafsi na Mungu na ndiye awe kipaumbele katika maisha yake. Na kama hatalichukulia kwa maanani jambo hili mwinjilisti hatamfahamu Mungu kwa kina. Hata kuwa katika uongozi wa Mungu na wala hatazaa kilicho sahihi,yaani matunda ya kiroho.

Tafadhali angalia mitazamo nane hii ya maombi ambayo inaweza kufanyika wakati tukiwa na Mungu kwa muda wetu wa Binafsi.

1. Sifa na Kuabudu

Biblia inasema katika Zaburi 48:1, “Bwana ndiye Mkuu, na mwenye kusifiwa sana...” Zaburi 34:1-3 inasema, “Nitamhimidi Bwana kila wakati, sifa zake zi kinywani mwangu daima, katika Bwana nafsi yangu itajisifu, wanyenyekevu wasikie wakafurahi, mtukuzeni Bwana pamoja nami na tuliadhimishe jina lake pamoja.”

Tunamsifu Mungu katika ibada zetu jumapili, lakini vipi katika mida zetu binafsi na Bwana kati ya Jumatatu hadi Jumamosi? Biblia inasema katika Zaburi 22:3, “Na wewe u mtakatifu uketiye juu ya sifa za Israeli.”

Kusifu ni nini? Kusifu ni kumwinua na kumtukuza Mungu kwamba Yeye ndiye. Shukrani ni asante kwa Mungu kwa kile alichotufanyia. Kusifu ni kutukuza sifa na ukuu wa Mungu.

Kibiblia, Kumsifu Mungu, ni mtu kutumia akili zake, hiari yake na hisia zake. Si vibaya kuwa na hisia wakati wa kumsifu Bwana. Kusema kwamba hii si kweli ni sawa na kusema kwamba mtu hawezi kutumia akili na matakwa yake. Mwanadamu ana mwili, na nafsi (akili zake, **matakwa** na **hisia**), na roho (I Wathesalonike. 5:23).

Hata hivyo, kuna aina mbalimbali za hisia na mihemuko. Muhemko ni kile kitendo cha mtu kupoteza hisia za mtu mwingine. Kama hii itatokea katika ibada, ibada itaanza kumomonyoka kutoka katika maandiko na utaratibu wake. Biblia haijakataza hisia katika kusifu lakini inakataa mihemuko.

Kuna ushauri kidogo wa jinsi mtu anavyoweza kumsifu Bwana katika muda wake binafsi na Mungu:

A. Imba Tenzi kwa kutumi a kitabu cha nyimbo au kitabu chocote cha kikristo.

Ukiwa na watu katika chumba unachokuwa na muda binafsi na Mungu unaweza kusoma maneno ya wimbo kwa Bwana kwa kutumia akili. Mfano mzuri wa kumsifu Mungu ni ule wimbo wa, “Baba, Mwana, Roho”.

Soma mistari ya mwanzo ya wimbo halafu simama, tafakari na tenda kulingana na maana ya maneno ya wimbo huo. Kumsifu Mungu kunatokana na kile ulichokisoma. Baada ya hapo, soma mstari wa pili na fanya kitu kilekile mpaka wimbo uishe. Katika mgawanyo wa nyimbo wa tenzi nyingi orodha ya nyimbo huoneshwa.

B. Imba au soma wimbo wa sifa

Biblia inasema katika Waefeso 5:19-20, “Semezaneni kwa zaburi, tenzi na nyimbo za kiroho. Imba na piga mziki kimoyomoyo kwa Bwana ukimshukuru Mungu Baba kwa kila kitu katika jina la Bwana.” Jua kwamba sifa ziko kimaandiko ni sahihi na kweli.

C. Soma sura za maombi katika Biblia na zitenge sura hizo

Zaburi 8:1 inasema, “Wewe Mungu Bwana wetu jinsi lilivyo jina lako duniani mwote wewe umeuweka utukufu wako mbinguni.”

Katika kuitenga mistari weka jina lako. Kwa mfano “Oh Bwana,”wangu” jinsi lilivyo jina lako duniani mwote wewe umeuweka utukufu wako mbinguni.” Soma kila mstari mara moja kama ulivyoona kwenye Biblia, na halafu soma tena kwa kuitenganisha ukimsifu Mungu kibinafsi.

Sura zingine katika Biblia ni nzuri sana katika sifa. Nazo ni: Zaburi 8,9,19, 24, 65, 92,104, 139, maombi ya Yesu na Paulo mtume na sura mbalimbali zilizo katika kitabu cha Ufunuo.

Jinsi nyingine bora za kutafuta sifa za kumsifu Mungu katika maandiko ni kutafuta neno lililo andikwa “Sifu” kwenye rejea na dondoo za maneno kwenye Biblia..

Sifa ni sehemu muhimu katka ukuaji wa kiroho wa mkristo. Soma Ufunuo 4 na 5 kujua kile tutakachokuwa tukikifanya mbinguni.

2. Kuungama

Siyo vizuri kutumia muda mwingi katika kuungama. Tunapotenda dhambi Roho Mtakatifu husema haraka sana kwa Mungu wetu kuhusiana na dhambi tuliyoifanya. Kuungama dhambi tunatakiwa kufanya pale tunapokuwa tumeelezwa na Roho Mtakatifu. Biblia inasema katika 1Yohana 1:9 kwamba “Tukiziungama dhambi zetu yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi na kutusafisha na udhalimu wote.”

Wakati wa muda Binafsi na Mungu, Roho Mtakatifu hutukumbusha dhambi ambazo hatujatubu. Labda anaweza kutukumbusha kwa njia yenye mtazamo mbaya, hasira au uchungu kwa watu. Kwa jambo hili tunapaswa kuziungama dhambi zetu zote.

3. Shukrani

Biblia inasema katika Wafilipi 4:6, “Msijisumbue kwa neno lolote bali katika kila neno kwa kusali na kuomba pamoja na kushukuru, haja zenu zijulikane na Mungu.”

Shukrani ni asante kwa Mungu kwa yake aliyotufanyia. Kwa mfano “Ninakushukuru Mungu kwa afya yangu, chakula changu na familia yangu.”

4. Kusikia sauti ya Mungu

Biblia inasema katika Zaburi 62:5 “Nafsi yangu humngoja Mungu peke yake, kwa kuwa tumaini langu hutoka kwake.” Zaburi 46:10 inasema, “Acheni mjue ya kuwa Mimi ni Mungu...”

Tunaisikiaje sauti ya Mungu? Mungu hutumia njia mbili kubwa kuzungumza na waumini wake kwa mambo ya kila siku: Roho Mtakatifu na Neno lake. Warumi 10:17 inasema, “Imani chanzo chake ni kusikia na kusikia huja kwa neno la Kristo.”

Biblia ni barua ya upendo kutoka kwa Mungu. Nia ya Mungu ni kuzungumza na kila mtu kila siku kupitia neno lake kwa njia ya Roho mtakatifu. Hapa kuna njia chache za kuisikia sauti ya Mungu:

A. Anza kwa kusoma kitabu katika Biblia, na tunashauri uanze na kitabu cha Waefeso.

B. Mwombe Mungu akupe ukweli wa Kiroho kwa kila mstari au sura. Kwa mfano Waefeso 1:1 inasema Paulo, mtume wa Yesu Kristo kwa mapenzi ya Mungu kwa watakatifu walioko Efeso waaminifu katika Kristo Yesu.” Mambo manne ya Kiroho ni:
   1) Paulo ni muumini na ni mtume wa Yesu Kristo.
   2) Alikuwa ni mtume, aliyechaguliwa kwa mapenzi ya Mungu.
   3) Neno “Watakatifu” linamaanisha Wakristo katika Efeso.
   4) Watu hawa walikuwa ni waaminifu kwa Yesu Kristo.

C. Zitenganishe kweli hizi za Kiroho. Mungu anazungumza na msomaji kupitia kweli hizi. kwa mfano Mungu ananieleza kweli nne katika Waefeso 1:1:
   1) Thomas Wade, wewe ni mwanafunzi wa Yesu kwa mapenzi yangu
   2) Thomas Wade, Nimekuchagua kwa mapenzi yangu.
   3) Thomas Wade, Ni mtakatifu unapoishi huko Belo Horizonte, Brazil.

4) Thomas Wade, Ninataka uwe mwaminifu kwa Yesu Kristo.

5. Omba neno la Mungu lirudi kwa Mungu

Tumia mistari katika kuomba. Kwa kutumia mistari hii katika Waefeso tunaweza kusema kwamba"Baba Mungu wangu ninakushukuru kwa sababu wewe Bwana umeniita kuwa mwanafunzi wa Yesu. Ninakushukuru Mungu kwa sababu mimi ni mtakatifu wako. Ni mtu niliyetengwa kwa ajili yako, Baba yangu nia yangu ni kuwa mtu mwaminifu kwa Kristo katika jina la Yesu ninaomba, Amen!"

Baada ya kupita katika hatua hizi na ule mstari wa kwanza, sasa endelea katika ule mstari wa pili na kufanya vivyo hivyo.

6. Maombezi

Biblia inasema katika Waefeso 6:18, "Kwa sala zote na maombi mkisali wakati wote katika Roho mkikesha kwa jambo hilo hilo na kudumu katika kuwaombea na watakatifu wote."

Maombezi ni maombi kwa ajili ya watu wengine. Watu wengi huwa wanakaratasi tupu mwishoni mwa Biblia zao. Igawe karatasi hii katika sehemu nane au tumia kijitabu cha notebook ili uandike majina ya watu unaotaka kuwaombea.

Kwa mfano, Kule juu ya karatasi andika neno "Kutwa" Na halafu andika jina la mke wako, watoto, wazazi, ndugu n.k. watu hawa ni wale walio karibu sana nawe.

Katika ukurasa unaofuatia andika neno" **Jumapili"**. Chini ya neno hili andika orodha ya watu utakaowaombea katika siku hii ya juma. Omba kwa ajili ya Mchungaji na mke wake, mwalimu wako wa shule ya Jumapili na wengine katika darasa lako.

Endelea katika kolamu nyingine ambapo utaandika neno "**Jumatatu**" hili ni eneo utakaloandika rafiki wa familia yako na marafiki wengine.

Ukurasa unaofuata utaandika pale juu kichwa cha habari "**Jumanne** katika siku hii omba kwa ajili ya watu walipotea.

"**Jumatano"** itakuwa ndiyo kichwa cha habari juu ya karatasi. Katika siku hii andika majina ya Wamisionari, viongozi wa jumuiya yako ya kanisa, viongozi wa kanisa lako au watu wengine unaotaka kuwaombea.

Katika ukurasa unaofuata andika neno **Alhamisi**. Katika ukurasa huu andika majina ya viongozi wa nchi yako. I Timotheo 2:1&2, "Ninashauri kwanza kabla ya yote kwamba haja, maombi, maombezi na shukrani zifanyike kwa kila mtu kwa mamlaka kwamba tuweze kuishi kwa amani na maisha mazuri katika utakatifu."

katika ukurasa unaofuata andika neno **Ijumaa**. Katika ukurasa huu andika majina ya wale unaowafahamu ambao wamerudi nyuma au hata kupotea kabisa.

Ukurasa unaofuata andika **Jumamosi.** Katika ukurasa huu andika majina ya marafiki, jamaa wa kanisani na hata huduma au miradi yako unayohusika nayo.

Ikiwa mwinjilisti atafanya hivi ataomba kwa ajili ya watu wengi kwa kila siku katika juma. Watu wengine wanaamini kwamba Warumi 16 ni orodha ya maombi ya Paulo kwa ajili ya Wakristo waliokuwa katika Rumi.

7. Kutafakari na Kumbukumbu ya maandiko

Biblia inasema katika Kitabu cha Yoshua 1:8, “Kitabu hiki cha torati kisiondoke kinywani mwako bali yatafakari maneno yake mchana na usiku upate kuangalia na kutenda sawasawa na maneno yote yaliyoandikwa humo maana ndipo utakapoifanikisha njia yako kisha ndipo utakapostawi sana.”

Mstari huu unasema kwamba kulitafakari neno la Mungu usiku na mchana kunasababisha maisha kubadilishwa. Warumi 8:29 inasema kwamba kusudi la Mungu ni kumfanya mwinjilisti awe katika sura ya Yesu Kristo. Matokeo yake ni mienendo inayofaa na maisha yenye kustawi. Swali ni, “Tunaritafakarije neno la Mungu usiku na mchana? Tunalitafakarije Neno wakati tumelala?”

A. Chagua mstari katika Biblia kila juma.
B. Usome mstari na yaliyomo.
C. Mwombe Mungu akuoneshe kweli za Kiroho katika mstari huo.
D. Uchanganue kila mstari katika maombi.
E. Andika mstari huu katika karatasi na kumbukumbu zake.
F. Wakati wa mchana, usome mstari huu mara nyingi. Fanya hivi katika sehemu ulipo au wakati wako wa ukimya lakini zingatia kuiangalia karatasi yako ya kumbukumbu hata mara tano kwa siku.
G. Kitu utakachokifanya cha mwisho wakati wa usiku ni kusoma mstari huu. Hii inafanyika ili upate kuuweka mstari huu katika fikra zako.

8. Unyenyekevu

Biblia inasema katika Waebrania 4:16, “Basi natukikaribie kiti cha neema kwa ujasiri ili tupewe rehema na kupata neema ya kutusaidia wakati wa mahitaji.

III. MWINJILISTI MASHUHURI NA WOKOVU

Desturi zako ndizo huendeleza matendo yako. Mathayo 12:34 inasema, “Maana kinywa cha mtu huyanena yaujazayo moyo wake”. Mwinjilisti anapaswa kuelewa msingi wa mafundisho ya Agano Jipya. Kile mwinjilisti anachokiamini katika Biblia, wokovu, huduma na kanisa ni mafanikio katika huduma yake. Kuamini kwake katika wokovu kunaleta picha ya ujumbe wake. Wakristo wengi hawajui kujibu maswali muhimu yanayohusiana na;

1. **Injili ni nini?** (Andika kwa kalamu ya penseli kulingana na vile unavyoelewa kutoka katika maandiko) Kuona maana ya neno Injili katika Biblia soma I Wakorintho 15:1-4.

_____
_____
_____
_____

2. **Nini maaa ya uzima wa milele?** (Andika jibu lako kwa kalamu ya penseli kulingana na vile unavyoelewa katika maandiko) Kuona maana ya neno uzima wa milele soma Yohana 17:3.

_____
_____
_____
_____

Ni vizuri kwa mwinjilisti kuelewa kwa usahihi maana ya wokovu kulingana na jinsi ulivyo katika Agano Jipya. Kwa kuwa Agano Jipya lina watu waliookoka, kwa hiyo mafundisho ya mwinjilisti yatakuwa ni msingi sana katika kazi yake.

Mwinjilisti hana kazi isipokuwa tu ni pale atakapoamini kwamba watu bila Kristo wamepotea milele na watakwenda Jehanamu milele. **Je ni kweli unaaini hivyo?** Mwinjilisti anapaswa aelewe kwamba mtu bila Yesu huyo ametengwa, na maisha yake amejawa na simanzi, woga, hukumu, upweke, na kwamba ana utupu mkubwa katika roho yake.

Kitu cha muhimu ni mafudisho ya hukumu ya mwisho. Kuna baadhi ya tamaduni bado zinaamini roho chafu na mafundisho ya watu waliokufa kwa nguvu sana. Yesu alitufundisha kuhusiana na ufufuo na si watu waliokufa. Katika Waebrania 9:27 inasema, “Na kama vile watu wanavyowekwa kufa mara moja na baada ya kufa hukumu.”

Luka 19:10 inasema kwamba Yesu alikuja kutafuta na kuokoa kilichopotea. Hili pia ni jukumu la mwinjilisti. Watu wanapotea hasa wanapotegemea vitu vingine ili kupata wokovu na kumwacha Yesu. Wagalatia 2:16 inasema,“hali tukijua ya kuwa mwanadamu hahesabiwi haki kwa matendo ya sheria bali kwa imani ya Kristo Yesu wala si kwa matendo ya sheria maaana kwa matendo ya sheria hakuna mwenye mwili atakayehesabiwa haki.”

Ni muhimu kwa mwinjilisti kuelewa kwamba mtu aliyepotea katika dhambi, hajaokoka bado na anapaswa kujiona kwamba amekwisha potea. Tusitamani kuona “watu waliompokea Kristo” badala yake tunatakiwa kuwafanya watu kuwa wanafunzi. Tunapaswa kuwaeleza watu juu ya kazi ya kanisa, kuwafundisha viongozi wenyeji, wajiongoze na kuwa na kanisa linalojizalisha na kuanzisha kanisa jingine kwa uongozi wa Roho Mtaakatifu.

Ni vizuri sana mtu kuelewa cha kufanya ili ajue jinsi atakavyoweza kuokoka. Mtu kuokoka ni pale atakapotubu dhambi zake na kuweka tumaini lake kwa Yesu kama Bwana na Mwokozi. Mwinjilisti anapaswa kufanya kila kinachowezekana ili watu wajue hali zao zote mbili ya kwamba wamepotea na wanapaswa kumkaribisha Yesu.

Kwanza- anapaswa atubu dhambi zake. Marko 1:15 Kutubu ni nini? Neno kutubu lina maana ya kugeuka na kumwelekea Yesu na kubadili mwelekeo wa akili na mawazo yako. Kubadili akili za mtu ni kugeuka kutoka katika dhambi na kumwendea Yesu inamaana kwamba mtu anakuwa akiendesha maisha yake menyewe na anaamua kumwachia Yesu ayaongoze. Kutubu ni kuacha dhambi zako na kumkabidhi Yesu Kristo maisha yako kama Bwana na mwokozi. Na hii imeoneshwa katika Warumi 10:9 mtu anapoamua kumkiri Yesu kama Bwana anageuka maisha yake na kuyakabidhi kwa Yesu kama Bwana.

Kutubu ni nini? _____

_____
_____

Pili- Anapaswa aweke imani yake kwa Yesu kama Bwana na mwokozi na mpatanishi. Neno "Kuamini" Katika Warumi 10:9 Ni zaidi hata ya kujua mawazo ya mtu kuhusu Yesu. Biblia inasema katika Yakobo 2:19 hata mapepo yana amini ukweli kuhusu Yesu.

Neno "Imani" au "Kuamini," katika kiyunani ni "Pistis." Hii inamaanisha kwamba mtu anatakiwa kutoa maisha yake kwa Kristo. Kitu chochote tofauti na Kristo si Imani ya kweli. Tatizo kubwa la watu wengi ni kwamba watu wengi wanaamini Historia ya Yesu na wanaweka katika akili zao. Kazi yetu ni kuwaonesha watu tofauti kati ya imani ya kweli na ile ya uongo

Imani ni nini? _____
_____

Imani iokoayo haitegemei kitu chochote ili kupata wokovu. Kwa mfano, mtu hapaswi kutegemea kazi zake, maisha mazuri, sanamu, bikra mariamu, malaika, watakatifu au sehemu fulani bali anatakiwa amtegemee Kristo ambaye ndiye mpatanishi, mwokozi na Bwana. Katika kitabu chake, Upandaji wa makanisa ya mahali, Chales Brock anasema, "maana ya wokovu ambayo haileti tiba ya dhambi, toba na amani inaweza kuzaa dini lakini siyo kanisa."

Kila mwinjilisti anapaswa kufuata maongozi ya Roho Mtakatifu kwa sababu yeye ndiye anayewaonesha wapotevu dhambi zao. Mwinjlisti anapaswa kueleza ukweli na injili kamili ya Yesu kwa nguvu ya Roho Mtakatifu anayetenda ndani ya watu ili apate kuzaa matunda yanayokaa.

III. MWINJILISTI MASHUHURI NA USHUHUDA BINAFSI

Kusudi la ushuhuda ni kushirikisha ufahamu binafsi. Inawezekana kujadili kuhusu vitu vilivyowahi kuwatokea watu lakini ni vigumu sana kujadili juu ya ufahamu wao. Katika Matendo 22:1-16 na Matendo 26:9-23, Mtume Paulo anaeleza juu ya historia yake jinsi alivyompokea Kristo na kile kilichotokea baada ya kumwona.

1. Miongozo ya kukumbuka katika kushirikisha ushuhuda wa Mtu

A. Eleza kwa ufupi (dakika 2 hivi).
B. kumbuka kwamba kusudi lako ni kuwaonesha waliopotea jinsi ulivyompokea Kristo. Injili itaelezwa baadaye.
C. Usihubiri.
D. Usieleze mpango wa wokovu wakati huu.
E. Usiite mwaliko.
F. Usitumie maneno ya kihuni. Kwa mfano "Nikabatizwa" wasioamini watafikiri kwamba ili kuokoka ni lazima ubatizwe. Ni vizuri kusema siku moja jioni nilimpokea Yesu moyoni mwangu au nilimwamini Yesu kama Mwokozi na Bwana wangu
G. Kama utapenda, tumia vifungu vya Biblia.
H. Andika ushuhuda wako. Usizidi maneno 250 hadi 350
I. Malizia ushuhuda wako kwa maneno haya:
    1) Sasa ninauhakika kwamba nina uzima wa milele.
    2) Je ungependa nikueleze kutoka katika Biblia jinsi ya kuwa na hakika ya uzima wa milele?

2. Ushuhuda

Jibu maswali yafuatayo ili kukusaidia jinsi ya kuandaa ushuhuda wako:

A. Maisha yangu yalikuwaje kabla ya kumjua Yesu, eleza mtazamo wako, maisha na dhambi. (Matendo 22:1-5 na 26:4-11)

B. Nilitambuaje kwamba namhitaji Kristo? (Matendo 22:6-8 na 26:12-15)

C. Wapi na ni namna gani nilimpokea Yesu?? (Matendo 22:6-10 na 26:13-18)

D. Nini tofauti ya maisha yangu kabla na baada ya kumpokea Kristo? (Matendo 22:10-21 na 26:19-23)

E. Hitimisho:

Hitimisha kwa kusema, “Sasa nina uhakika wa uzima wa milele. Je mngependa niwaeleze Biblia inasemaje namna ya kuwa na uhakika wa maisha ya Milele?”

Ulichokifanya ni kwamba umejenga daraja kati yako na waliopotea. Sasa unakuwa unaomba ruhusa ya kupita katika daraja na uingie katika maisha yake binafsi. Anaweza kusema “ndiyo” au “hapana”. Kama

atakubali mweleze habari njema. Kama atakataa mwombe.Kama atakubali, andika jina lake kwenye karatasi yako ndogo ya kumbukumbu, ili iwe kumbukumbu ya kumwombea kila wakati.

V. MWINJILISTI MASHUHURI NA UINJILISTI BINAFSI – MISTARI SITA INAYOIELEZA INJILI

Kuna tamaduni mbili:

1. Watu wasio Wakristo
2. Wakristo

Kuna misingi maalumu ya injili bila kujali ni tamaduni gani. Utamaduni hauwezi kuigeuza injili. Kweli hizi muhimu zinapaswa kushirikishwa kwa namna fulani kabla mtu hajampokea Kristo. Tunashauri unashirikisha kwa njia ya masomo ya Biblia ya muda mrefu au kwa njia ya hadithi. Bila kujali mtu anaweza kutumia namna ipi katika kuwakilisha kweli, anachotakiwa nikujua misingi ya kweli halisi ya Injili.

Maswali kwa wasio Wakristo

Katika jambo hili unatakiwa uanze kwa maswali ya msingi kama vile, “Unamwelewaje Mungu na Yeye ni nani?” Msikilize na muulize kama unaweza kufanya masomo ya Biblia pamoja naye. Katika jamii ya wasioamini unaweza kumuuliza kama angependa kujifunza juu ya Mungu muumbaji ambaye aliumba ulimwengu na jinsi anavyoweza kumjua kibinafsi.Tumia masomo rahisi ya Biblia au habari za matukio ya kibiblia.

Maswali kwa Wakristo

“Ninaweza kukuuliza swali? Ikiwa utakufa usiku unajua kwamba unao uzima wa milele na kwamba utakwenda mbinguni?” (Jikumbushe swala hili). Ikiwa hatajibu vizuri basi endelea kwa kumpa ushuhuda wako na mweleze habari njema. Ikiwa atajibu “Ni na uhakika” sasa muulize swali hili ambalo ni la pili “hebu fikiri kwamba sasa ungekuwa mbele za Mungu na akakuuliza kwa nini nikuruhusu uingie mbinguni?” (Mkumbushe swali hili tena) ungelimjibuje? Kama hatajibu mweleze habari njema. Swali jingine ambalo unaweza kulitumia “je una ushirika na Yesu Kristo au je uko katika hatua ya kufanya ushirika naye?”

ANGALIZO: Swali la milele la Wahindu, Wabuda linatakiwa liwe la tofauti kabisa na lile la Wakristo kama vile la Waroma. Katika madhehebu ya tamaduni hizi neno lolote lililo na matumizi ya Mungu, Yesu, mbinguni, au jehanamu linatakiwa litumike kulingana na mtu wa tamaduni aliyo nayo. Kwa mfano kumwelezea Mungu kwamba yeye ndiye muumbaji wa vitu vyote ni mwanzo mzuri wa kumtambulisha Mungu ni nani. Maisha ya Yesu na makusudi yake yanatakiwa kuelezwa tunapo mhusisha tu.

Mfano mzuri tena mwingine ni neno “mbinguni” neno hili kwa Wabuda ni kuachana na tamaa zote. Kwa wahindi lina maana ya kutoabudu wafu. Kwa waanimist linakuwa na maana nyingi na inaweza kuwa ni kutofautishwa na kuzimu.

Kwa tamaduni nyingi Biblia siyo kitabu ambacho watu wanakijali. Watu wengi hasa kwa wale ambao bado hawajafikiwa yamkini anaweza kuwa hawajawahi kusikia kitu Biblia. Unachokifanya ni kuwaeleza watu kwamba Biblia ni kitabu ambacho Mungu ametupa ili apate kujifunua kwetu. Hawaamini hii. Lakini ikiwa watapenda kujifunza pamoja nawe Roho Mtakatifu ataanza kujifunua na kuwaonesha ukweli.

Usiwe na mashaka juu ya Biblia kwamba ni neno la Mungu au hapana. Onesha kwamba imani yako iko katika unachokiamini, kimeandikwa katika kitabu cha neno la Mungu na kwamba unapenda useme nao. Ni vema mwinjilisti akatafuta kifaa kinachofaa kwa ajili ya kushuhudia watu anaowaongoza.

UKWELI WA INJILI HAUBADILIKI LAKINI MITAZAMO HUBADILIKA KULINGANA NA UTAMADUNI

KUMBUKA: Katika jamii ya kikristo unaweza kuendelea kutumia maswali ya milele. Lakini katika jamii ya wasio amini utatakiwa kutumia utambuzi katika kutambua kiwango cha uelewa wa kiroho. Uelewa wa mtu katika neno kama vile mbinguni linaweza kuwa ni tofauti na lile la kwenye Biblia.

Kuiwakilisha Injili

(Mistari sita inayoeleza ukuu wa injili.)

1. Kusudi la Mungu katika maisha yako

Biblia inasema katika I Yohana **5:13, "Nimewaandikia ninyi mambo hayo ili mjue ya kuwa mnao uzima wa milele ninyi mlioliamini jina la Mwana wa Mungu."**

Kusudi la mstari: Mungu anataka kutupa hakika ya maisha ya milele kwa sababu ya upendo wake kwa mwanadamu.

Maelezo ya mstari: Maisha ya milele ni vitu viwili:

a) Kumjua Yesu na kuwa na amani yake ktika moyo wako wakati ukiwa katika maisha haya. (Yohana 17:3)
b) Kuishi na Yesu Kristo mbinguni milele baada ya kufa (Yohana 14:1-3)

Matumizi ya Mstari: Unatakiwa kujua kwa uhakika kwamba unao uzima wa milele ?

Angalizo: Kwa Wakristo na wasio Wakristo maelezo haya yanatakiwa kuwa wazi kimaelezo na inaweza kukuchukua muda.

2. Hitaji lako

Biblia inasema katika **Warumi 3:23**, **"Wote wamefanya dhambi na kupungukiwa na utukufu wa Mungu".**

Kusudi la mstari huu: Ni kuonesha kwamba wote wana dhambi.

Maelezo ya mstari: Dhambi ni nini? Dhambi ni kutomtii Mungu. Kwa mfano, wote sisi tumefanya dhambi kama vile uongo, hasira, urafi, majivuno n.k.

Matumizi ya mstari huu: Unatambua ya kwamba umefanya dhambi na ni nini madhara ya dhambi?
Biblia inasema katika warumi **6:23, "Mshahara wa dhambi ni mauti bali karama ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu."**

Kusudi la mstari: Unaonesha kwamba wote tunastahili mauti kwa sababu tumetenda dhambi.

Maelezo ya Mstari: mauti ni nini? Ina maana ya kutengana na Mungu katika njia mbili.

Kwanza, mauti ni kutengana na Mungu sasa katika maisha ya duniani hapa. Ni maisha yasiyo na furaha au amani katika Roho. Ni maisha yasiyo na uhakika wa uzima wa milele na bila Yesu katika roho yako. Utengano wa Mungu humwacha mwanadamu akiwa tupu na roho yenye woga.

Pili, mauti ni utengano na Mungu milele katika jehanamu. Haya ni maisha bila Yesu milele yote. Kulingana na Biblia sisi sote tunastahili mauti, na kutengana na Mungu kwa sababu ya dhambi zetu.

Matumizi ya Mstari: Unaelewa kwamba unastahili kufa kwa sababu ya dhambi zako?

3. Pendo la Mungu

Biblia inasema katika Warumi **5:8, "Bali Mungu aonesha pendo lake kwetu sisi wakati tungali wenye dhambi, Kristo akafa kwa ajiri yetu."**

Kusudi a mstari: kuonesha kwamba Mungu anatupenda sana hata akamtoa mwana wake Yesu Kristo akafa kwa ajiri ya dhambi zetu.

Maelezo ya mstari: Mshahara wa dhambi ni mauti. Yesu Kristo aliadhibiwa akahukumiwa na kuuawa msalabani ili alipe gharama ya dhambi zetu.
Kifo cha Yesu kilikuwa ni dhabihu kamili ili kumweka huru mwanadamu kutoka katika dhambi. Watu wengi wanajaribu kumfikia Mungu kwa njia nyingi: wakitegema kazi zao, maisha yao mazuri, Wanajaribui kumfikia Mungu kwa njia ya utakatifu, sanamu, michoro, roho chafu na wafu. Juhudi za mwanadamu hazina nguvu za kutakasa dhambi yake. Njia ya kuweka ushirika na Mungu ni kupitia Yesu tu. Baada ya Yesu kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu, alifufuka kutoka wafu akayashinda mauti. Yu hai na anataka aingie na kuishi katika maisha yako.

Matumizi ya Mstari huu: Unaamini kwamba Yesu ni Bwana wako, Mwokozi na mpatanishi?

4. Jukumu lako

Biblia inasema katika Warumi **10: 9, "Kwamba ukimkiri Yesu kwa kinywa chako na kuamini moyoni mwako ya kwamba Yesu ni Bwana na kwamba Mungu alimfufua katika wafu utaokoka."**

Kusudi la mstari: Ni kukuonesha cha kufanya ili upate kumpokea Yesu kama Bwana wako
Maelezo ya mstari: Kumpokea Yesu unatakiwa kufanya mambo mawili:

a) Kwanza, Kumpokea Yesu unapaswa kukiri kwamba yeye ni Bwana wako tu. Uzikatae dhambi zako na ugeuke kumfuata Yesu. Hii inamaana kuacha kuendesha maisha yako na kumpa Yesu. Na hii ni toba
b) Pili, kumpokea Yesu unapaswa kuamini moyoni mwako kwamba Yesu alifufuka katika wafu na kwamba yeye ni mwokozi wako. Ina maana kwamba unapaswa kuacha kuamini mambo mengine kama vile kazi nzuri,vinyago, sanamu, utakatifu au wafu na uweke imani yako kwa Yesu kama Mwokozi wako .

Matumizi ya Mstari: Uko tayari kumkiri Yesu kama Bwana na mwokozi wako na umkabidhi maisha yako kama Bwana? Je uko tayari kuacha kuabudu vitu vingine na umpe Kristo maisha yako sasa kama Bwana na Mwokozi wako?

Biblia inasema katika Warumi **10:13, "Atakayeliitia jina la Bwana ataokoka."**

Kusudi la mstari: Ni kuonesha kwamba yeyote atakayeliitia jina la Bwana ataokoka.

Maelezo ya Mstari: Unaweza kumpokea Yesu sasa kwa imani katika moyo wako.

Matumizi ya mstari: Uko tayari kumkabidhi Yesu na umwombe aingie katika maisha yako sasa? Kama uko tayari sema sala hii kwa moyo wako mbele za Mungu.

> "Bwana, Mimi ni mwenye dhambi, ninakuamini Bwana, kama Bwana wangu tu, mwokozi na mpatanishi, ninayatoa maisha yangu kwako. Ingia katika moyo wangu na uniokoe sasa, nigeuze na uyaongoze maisha yangu yote. Amen."

Unaamini kwamba Yesu amejibu maombi yako? Umeokoka?

MPANGO

HATUA ZA KUANZA

KANISA JIPYA

MPANGO

Sehemu hii inatoa muhtasari wa mchakato ambao mwinjilisti mvumbuzi atapaswa kufuata, mifano minne ambayo yaweza kutumika kuunda kanisa na pia miduara minne yenye undani wa kuanzisha kanisa kwa njia ya kuzidisha.

KUMBUKA: Huu si mpango wa kufuata.Hizi ni kanuni zinazotoa mwongozo wa mkakati gani mtu anaweza kuuanzisha. Lakini katika huduma inaweza kuwa tofauti. Cha muhimu ni kufuata uongozi wa Roho Mtakatifu kwa kadri anavyowainua viongozi wapya na kuwafunza kwa ajili ya kazi mpya pia atafungua milango.Kamwe usisahau kuwafunza wengine na wengine kuwafunza wengine, nk.

I. Mifano minne ya kuunda kanisa

II. Miduara ya Uinjilisti uvumbuzi

MIFANO MINNE YA KUUNDA KANISA

AWAMU 1.Katika kuanzisha kanisa ni kuanza chini kabisa kwenye hakuna hadi kufikia kanisa kuanza kuonekana. **AWAMU II** utaanza kuumba kazi mpya. Kuna mifano mingi sana ya kuanzisha kazi mpya lakini sasa tunakwenda kutaja minne tu. Sura hii pia inatoa mpango kwa AWAMU I

1. KANISA LA KIMAPOKEO

Aina hii ina msingi ulioratibiwa. Hii mara nyingi ina ratiba kama vile shule ya Jumapili. Hii zaidi ni ya Kibiblia. Kuna mkazo mkubwa juu ya kuwa na jengo ambalo mara nyingi linasimamiwa na mchungaji au kikundi cha wazee au mashemasi.

2. KANISA LA SATELLITE

Aina hii ya kanisa kwa upana lina makanisa mama kama mdhamini ambapo watakuwa na watu waliotumwa kusaidia kazi na/au watu waliokusanyika kumwabudu Mungu. Kanisa mama au kanisa mfadhili watasimamia misheni hizi au/ na mikusanyiko ya ibada. Kila mkusanyiko utakuwa na ibada; Masomo ya Biblia; Ushirika n.k. katika manyumba; mbele za maduka au kanisa dogo. Hata hivyo bado ni washiriki wa kanisa mama. Mara zote sadaka na matoleo zinatumwa kwa kanisa mama. Tatizo kubwa ni kwamba mengi ya makanisa haya hayana utaratibu wa kujizalisha wenyewe mpaka yanakuwa yenyewe makanisa mama yaliyotengenezwa. Kwa mara nyingi matakwa yanayoongoza ni kwamba kanisa lazima liwe na ardhi, jingo na mchungaji aliyewekewa mikono. Walakini; haya ni matakwa yaliyotengenezwa na mwanadamu na hayatoki kwa Mungu.

3. KANISA LA VIKUNDI

Aina hii ni wakati ule kanisa mama litakuwa na vikundi vinavyokutanika majumbani; mabarazani na ofisini n.k. vikundi hivi vinatengenezwa kwa misingi ya kijiografia au kwa misingi ya jinsi moja ya uangalifu kama vile kundi la vijana, kundi la wanawake, kundi la wanaume n.k. mkazo katika mikutano ya vikundi ni jamii na maisha ya mwili; chini ya uangalizi na usimamizi wa mchungaji na washiriki. Hufanya huduma ya chakula cha Bwana katika kundi na hata hufanya ubatizo kwenye ngazi ya vikundi. Mlei atakayefanya haya maagizo anaongoza kila kundi. Kila juma vikundi vyote hukusanyika kwa ibada kubwa kuliko ya kawaida ya kutukuza.

4. KANISA LA POUCH

Mmisheni Curtis Sargaent aliukuza mtindo huu. Makanisa madogo madogo yanaanzishwa katika makao ya waumini wapya. Yote yanaongozwa na walei na kukua kufikia kiwango cha watu 15 na ndipo wanajizidisha. Kila kundi dogo ni kanisa dogo la mahala pale lililohuru na kujitenga.

POUCH ina maana:

P = **KUSHIRIKI –** Wana kikundi wote wanashiriki katika kujisomea Biblia; Ibada na maisha ya mwili.

O = **UTII** – Hiki ni kipimo cha kawaida cha mafanikio na siyo jinsi ukubwa wa kanisa linavyokuwa

U = **VIONGOZI WASIOLIPWA** – Viongozi wote na wachungaji ni watu wale wa kawaida.(wanaofanya kazi si kwa kulipwa)

C = **VIKUNDI**– Wanakutana katika vikundi vidogo vidogo.

H = **NYUMBA** – Huduma za ibada zinafanyika katika nyumba

MZUNGUKO/MDUARA WA UINJILISTI WA KI-UVUMBUZI

MZUNGUKO/MDUARA WA KWANZA.



MZUNGUKO WA UINJILISTI WA KI-UVUMBUZI
MZUNGUKO WA PILI



MZUNGUKO WA PILI UNAENDELEA

Ibada hii ya kusherehekea inaweza kuunganishwa na ibada ya sherehe ya mzunguko wa kwanza/au kuwa kanisa la mahali peke yake.



MZUNGUKO WA TATU



Katika mzunguko wa tatu; vikundi vya Habari Njema: Ibada za sherehe na mafunzo ya uinjilisti na uanafunzi sharti iongozwe na waumini wapya waliompokea Yesu katika mzunguko wa kwanza na wa pili badala ya viongozi waanzilishi.

MZUNGUKO WA TATU UNAENDELEA



MZUNGUKO WA NNE



Viongozi wenyeji sasa wanaongoza makundi yote ya habari njema na makundi ya Ibada za sherehe na ufuasi.Viongozi wapya sasa wanapaswa kufunzwa namna ya kuongoza kanisa.

MZUNGUKO WA NNE UNAENDELEA



Haya yanaweza kuwa kanisa moja au makanisa manne tofauti kwa kutegemea na mazingira halisi ya mahali.Viongozi wenyeji yawapasa kuongoza mizunguko yote hii.

MZUNGUKO WA TANO



Kanisa Jipya linajizalisha lenyewe.

KUTUMIA MKAKATI WA UINJILISTI UVUMBUZI KATIKA KUANZISHA MAKANISA YA VIKUNDI.



KUTUMIA UINJILISTI WA KI-UVUMBUZI KWA KANISA LA P.O.U.C.H.



MCHAKATO WA "OIKOS"

+ Watu ambao wamempokea Yesu kutokana na kubadilika kwa mtu wa amani bado hajawa muumini.



KWA NYONGEZA

MWINJILISTI MVUMBUZI NA JINSI YA KUONGOZA MASOMO YA BIBLIA MAJUMBANI BILA KUWA NA VIFAA……88

MWINJILISTI MVUMBUZI NA JINSI YA KUONGOZA MASOMO YA BIBLIA MAJUMBANI BILA KUWA NA VIFAA.

-Na Thomas Wade Akins.

Ufunguo wa kusoma na kujifunza neno la Mungu ni Roho Mtakatifu.Yesu alisema katika Yohana 16:13-14**, "Lakini yeye atakapokuja huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo atawapasha habari yake.Yeye atanitukuza mimi, kwa kuwa atatwaa katika yaliyo yangu na kuwapasha habari."**

Yesu Kristo ndiye kweli na Roho Mtakatifu ndiyo aidhihirishaye hiyo kweli ndani ya moyo wako. Je umewahi kuwa ukisoma Biblia na ghafla kifungu cha maandiko kinakuingia moyoni na Roho wa Mungu anasema nawe juu ya ukweli wake? Hii imewahi kunitokea mimi mara nyingi sana. Wakati nilipokuwa nikipita katika mapito magumu na wakati mugumu.Nilikuwa katika dimbwi la giza totoro.Na chini ya hilo giza kulikuwa na nuru, nuru yenyewe ni ya Yesu kristo. Nilianza kusoma neno ili nipate neno toka kwa Mungu.

Nilianza kusoma kitabu cha Isaya, na nilisoma sura ya 43 Roho wa Mungu ghafla akaniangazia ndani ya moyo wangu, mstari wa pili unaosema, **"Upitapo katika maji mengi nitakuwa pamoja; nawe; na katika mito, haitakugharikisha; uendapo katika moto hutateketea; wala mwali wa moto hautakuunguza…"**

Mungu aliposema nami juu ya ukweli huu moyo wangu ulifurikwa na amani. Japo bado ninazo siku nyingi za kutembea katika giza na majaribu ya moto, lakini najua kuwa sitaungua kwa kuwa Mungu amesema nami ukweli wake.

Ni muhimu kwa kiongozi kujua kuwa hafundishi masomo ya Biblia bali anaongoza watu kujifunza masomo hayo.Anaongoza katika njia ambayo mshiriki anapaswa kushiriki.Hasomi yeye kifungu lakini anaomba mtu mmoja katika kundi kusoma, Hawaambii kweli zilivyo katika kifungu, bali anauliza maswali ili kulisaidia kundi kugundua kweli hizo.Hatumii kifungu kwa ajili yao bali anawauliza wao kutoa mawazo juu ya namna ya kukifanya kifungu kiwe kama kinamzungumzia yeye/wao.

Tunapoongoza kikundi katika masomo ya Biblia, lengo letu ni kumsikia Mungu akisema nasi kupitia neno lake.Kama kiongozi wa kundi,kiongozi anapaswa kupitia hatua zifuatazo kabla ya kukutana na kundi.Utakapokuwa ukisoma Biblia peke yake, Mungu atasema nawe kweli ambazo angependa kusema na kundi.Kwa maelezo zaidi juu ya kusoma Biblia soma sehemu ya kitabu ambayo inazungumzia juu ya "Kusikia sauti ya Mungu" ukurasa wa 62.

Ningependa kupendekeza yafuatayo:

Hatua 1. Kiongozi wa kundi atachagua aya ya kujifunza. Anaweza kuanza na kifungu cha kwanza cha kitabu na kusoma kila mstari wa kila sura. Kwa mfano, unaweza kuanza na Injili ya Yohana, sura ya kwanza na mstari wa kwanza..

Hatua 2. Kiongozi atamwomba mmoja katika kundi kusoma kifungu cha kwanza.

Hatua 3.Kiongozi atakisoma tena kifungu akitumia lugha rahisi na ya kisasa.Kwa lugha nyingine ni kuwa atairahisisha zaidi: atairudia kauli katika hali rahisi zaidi.

Hatua 4. Baada ya kusoma kifungu, kisha kiongozi atauliza maswali ili kuutafuta ukweli katika kifungu hicho.Uliza maswali kama haya: nani, nini, lini, wapi, kwa nini na kwa jinsi gani.

Uliza aina hii ya maswali:

1.Kifungu hiki kinasema nini kuhusu Mungu?
2.Kifungu hiki kinasema nini kuhusu Yesu?
3.Kifungu hiki kinasema nini kuhusu dhambi?
4.Kifungu hiki kinasema nini kuhusu utii?

5.Kifungu hiki kinasema nini kuhusu mimi?
6.Kweli ya kiroho au kweli za kiroho ni zipi katika kifungu hiki?

Hatua 5. Kisha kiongozi atawaonyesha kundi aya zingine au vifungu katika Biblia ambavyo vinarandana na ukweli uliodhihirishwa katika vifungu hivyo. Kwa lugha nyingine waonyeshe kundi aya zingine katika Biblia ambazo zitafafanua na kuwaangazia kweli katika kifungu.

Hatua 6. Kisha kiongoza atapaswa kukitumia kifungu.Kifanye kifungu kuwa kama kinakuzungumzia wewe kwa kuweka jina lako na viwakilishi vya nafsi katika kifungu hicho.Zungumzia kila kifungu katika hali ya nafsi hai.Uliza kila mtu maswali haya. Je ukweli huu unakuhusu kwa namna gani? Je Kifungu hiki kinakuambia nini wewe binafsi? Na kila mtu ajibu peke yake.

Hatua 7. Baada ya kufuata utaratibu huu kwa kifungu cha kwanza, endelea na kifungu cha pili na tumia njia hii kujifunza kila kifungu hadi kitabu kizima.

Hatua 8. Mwisho wa kujifunza/somo waongoze kundi kwa maombi na muombee zile kweli za kiroho mlizozigundua wakati mkisoma aya hizo.

MFANO
Hatua 1:Chagua kitabu au aya. Kwa ajili ya kusudi letu tutachagua kitabu cha Injili ya Yohana.

Hatua 2:Uliza mtu mmoja katika kundi kusoma kifungu. **Yohana 1:1, "Hapo mwanzo palikuwapo Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu".**
Hatua 3: Fafanua kifungu.Kifungu hiki kinasema kuwa hapo mwanzo alikuwapo muumbaji, naye alikuwa kwa Mungu na alikuwa Mungu.

Hatua 4: Maswali:

1 Kifungu hiki kinasema nini kuhusu Mungu? Yeye alikuwepo toka mwanzo.Naye ndiye Mwanzo. Naye ni Neno.
2 Je kifungu hiki kinasema nini kuhusu Yesu?Ukisoma kifungu cha 14 utaona kuwa Neno ni Yesu.Kwa hiyo Yesu Kristo ni Mungu.

Hatua 5:Soma vifungu vingine vinavyorandanarandana.Yohana 1:14 inasema, **"Naye neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli."**

Uliza maswali mengi kwa kadri utakavyoweza kufikiri na waruhusu wanakikundi wajibu si kiongozi.
1.Nani alifanyika kuwa mwili? Yesu
2.Nani aliyekaa kwetu?Yesu.
3.Nani aliona utukufu wake? Yohana, mtu aliyeandika kitabu hiki.
4.Yohana aliona nini kwa Yesu? Utukufu wake.
5.Utukufu wake una maana gani? Ina maana ni wenye ukuu na heshima.
6.Ni kitu gani kingine Yohana aliona kwa Yesu? Alikuja toka kwa Baba.
7. Ni kitu gani kingine Yohana aliona Kwa Yesu? Alikuwa amejaa neema.
8. Neema ni nini?Neema ni Mungu kututendea mambo ambayo hatukustahili.Yesu ni neema.
9. Kweli ni nini?Kweli ni kinyume cha uongo.Yesu amejaa ukweli ndani yake na kila jambo asemalo.

Hatua 6. Kitumie kifungu, Kifungu hiki kinatufunza nini?Ni kweli zipi za kiroho zilizo katika kifungu hiki? Zifanye kuwa katika nafsi.Kiongozi awaruhusu kundi kujibu.

Baadhi ya kweli katika kifungu
1. Mungu alikuwepo toka mwanzo.
2. Hana mwanzo wala mwisho.
3. Ni wa milele
4. Yesu ni Mungu
5. Yesu ni muumbaji wa ulimwengu
6. Yesu aliniumba mimi
7. Yesu amejaa neema na kweli.Yesu alinipatia kile nisichostahili.Yesu hunifundisha kilicho kweli.(kumbuka kutumia viwakilishi vya nafsi).

Hatua 7. Soma kifungu kinachofuata na tumia hatua hizi hizi. Endelea na hatua hizi hadi kitabu kizima juma baada ya juma.Baada ya kumaliza kitabu cha Yohana, kisha chagua kitabu kingine na utumie mbinu hiyo hiyo.

Hatua 8. Funga kwa maombi lakini ombea zile kweli za kiroho zilizodhihirishwa kwako na kundi kwa ujumla kutoka kwenye aya mliyosoma.
Kuna vitabu vingi ambavyo vinaweza kukupa mwongozo wa kufunza masomo ya Biblia.Lakini pia ni vizuri kutumia Biblia pekee, kwa kuuliza maswali ambayo yamekuwa yakiulizwa hapa na mengine ambayo Roho wa Mungu atakuongoza.Usiache kuongoza masomo ya Biblia eti kwa kisingizio cha kukosa vifaa au vitabu vya rejea. Igundue furaha ambayo Roho wa Mungu atakuvuvia na kuuangaza moyo na kweli zake.